

Dozi za Kuimarisha Kinga Dhidi ya COVID-19

Je, dozi ya kuimarisha kinga ni nini?

Dozi ya kuimarisha kinga ni dozi inayotolewa baada ya mtu kupokea chanjo kamili. Kinga ya mwili huwa thabiti baada ya mtu kukamilisha kupokea chanjo; hata hivyo, huanza hudhoofika baada ya muda. Dozi ya kuimarisha kinga hutolewa ili kukulinda dhidi ya maradhi na kuongeza muda wa kinga inayotokana na chanjo uliyopokea.

Utoaji wa dozi ya kuimarisha kinga ulianza awali. Watu wengi nchini Marekani huenda wamewahi kupokea dozi ya kuimarisha kinga kupitia chanjo zinazopendekezwa mara kwa mara (kwa mfano, polio, pepopunda).

Je, ni nani anaweza kupokea dozi ya kuimarisha kinga?

Kituo cha Kudhibiti Magonjwa (CDC) kinapendekeza dozi moja ya Pfizer ya kuimarisha kinga dhidi ya COVID-19 miezi sita baada ya kupokea chanjo ya awali ya Pfizer dhidi ya COVID-19 kwa watu wafuatao:

- Walio na umri wa miaka 65 na zaidi
- Wanaoishi katika makao ya utunzaji ya muda mrefu
- Walio na umri wa kati ya miaka 50-64 na wana [matatizo mengine ya kiafya](#) (saratani, ugonjwa sugu wa figo, ugonjwa sugu wa mapafu, dimenshia, kisukari, Down's Syndrome, matatizo ya moyo, Ukimwi, kinga dhaifu ya mwili, ugonjwa wa ini, unene kupita kiasi, ujauzito, ugonjwa wa seli za damu, mvutaji sigara wa sasa au wa zamani, matatizo ya viungo/upachikaji wa tishu mwilini, kiharusi, matatizo yanayotokana na mihadarati)

CDC pia inapendekeza kuwa wafuatao wanaweza kupokea dozi moja ya Pfizer ya kuimarisha kinga mwilini baada ya kutathmini manufaa na hatari za dozi hiyo kwa watu hawa:

- walio kati ya miaka 18-49 na wana [matatizo mengine ya kiafya](#)
- watu wenye umri wa miaka 18-64 ambao wako katika hatari zaidi ya kuambukizwa COVID-19 kutokana na mazingira ya kazini au katika taasisi

Je, kwa nini dozi ya kuimarisha kinga dhidi ya COVID-19 inapendekezwa?

[Ufanisi wa chanjo](#) ya COVID-19 dhidi ya maambukizi (kuonyesha dalili za COVID-19) umepungua baada ya muda na huenda pia kutokana na virusi vya aina ya Delta. Ufanisi wa chanjo umesalia kuwa juu dhidi ya maambukizi hatari (yanayosababisha kulazwa hospitalini au kifo), lakini umeanza kupungua kwa walio na miaka 65 na zaidi.

Data kutokana na [uchunguzi wa kimatibabu](#) uliofanywa na Pfizer inaonyesha kuwa mtu anaweza kukabiliana na magonjwa kwa ufanisi zaidi baada ya kupokea dozi ya kuimarisha kinga, hivyo huenda dozi hiyo ikakuinga zaidi dhidi ya COVID-19. Pia, [data](#) kutoka Israeli inaonyesha kuwa dozi ya Pfizer ya kuimarisha kinga hupunguza maambukizi na magonjwa sugu. Data kutokana na uchunguzi wa

kimatibabu na kutoka Israeli inaonyesha kuwa athari za dozi ya kuimarisha kinga ni sawa na zinazotokana na dozi ya pili.

Je, ni wafanyakazi wepi wako katika hatari zaidi ya kuambukizwa COVID-19?

- Wanotoa huduma muhimu (wahudumu wa afya, wazima-moto, polisi, watunzaji)
- Wafanyikazi katika sekta ya elimu (walimu, wafanyikazi wasaidizi, wahudumu katika vituo vya chekechea)
- Wafanyikazi katika sekta ya chakula na kilimo
- Wanaofanya kazi viwandani
- Maafisa wa jela
- Wafanyakazi wa Posta Marekani
- Wafanyikazi wa uchukuzi wa umma
- Wafanyakazi wa duka la vyakula

Je, ninahitaji kuthibitisha taaluma yangu au kuonyesha kuwa nina matatizo ya kiafya ili niweze kupokea dozi ya kuimarisha kinga?

La. Unahitaji tu kusema taaluma yako au kutaja matatizo uliyo nayo ya kiafya ili upate dozi ya kuimarisha kinga.

Je, waliopokea chanjo zingine za COVID-19 wanaweza kupewa dozi?

Kwa sasa hakuna data ya kutosha kubaini ikiwa waliopokea chanjo zingine za COVID-19 wanahitaji dozi ya kuimarisha kinga dhidi ya COVID-19. Kwa sasa, waliopokea chanjo ya Moderna au Johnson & Johnson **hawapaswi** kupewa dozi ya kuimarisha kinga.

Naishi kwingine. Je, naweza kupewa dozi ya kuimarisha kinga?

Watu wengine huenda wakahitaji kupokea dozi ya kuimarisha kinga baadaye. Idara ya Afya ya North Dakota itawasiliana na wanaohitaji dozi wakati huo ukifika.

Je, hii inamaanisha kuwa chanjo za COVID-19 hazifanyi kazi?

Kupendekezewa dozi hii hakumaanishi kuwa chanjo za COVID-19 hazifanyi kazi. Idadi ya wanaolazwa hospitalini iko [juu zaidi ya mara 10-22](#) kwa watu wazima ambao hawajapata chanjo. Uwezekano wa waliopokea chanjo kugonjeka kutokana na COVID-19 uko [chini mara tano](#) ikilinganishwa na wale ambao hawajachanjwa. Ufanisi wa chanjo umepungua dhidi ya maambukizi (kama vile kuwa na dalili za COVID-19 licha ya kupokea chanjo) lakini bado chanjo inazuia vifo na kulazwa hospitalini. Ufanisi wa kuzuia kulazwa hospitalini umepungua kwa walio na umri wa miaka 65 na kuendelea.

Je, dozi ya kuimarisha kinga ni tofauti na dozi ya ziada?

Ndiyo, watu walio na [kinga hafifu](#) na hapo awali walipokea chanjo ya Pfizer au Moderna dhidi ya COVID-19 wanahimizwa kupokea dozi ya ziada ya chanjo ya Pfizer au Moderna. Dozi ya ziada hutolewa angalau siku 28 baada ya kukamilisha dozi ya kwanza. Watu walio na kinga hafifu hawawezi kulindwa kikamilifu kwa kupokea chanjo za mwanzo pekee na wanahitaji dozi tatu ili kinga yao iimarike.

Je, ninahitaji dozi ya kuimarisha kinga ikiwa nimepokea chanjo kamili?

La. Kwa madhumuni ya afya ya umma, watu wanachukuliwa kuwa wamechanjwa kikamilifu wiki mbili baada ya kupokea dozi mbili za chanjo ya Pfizer au Moderna dhidi ya COVID-19 au dozi moja ya chanjo ya Johnson & Johnson ya COVID-19.

Je, ninaweza kupata chanjo wapi?

Maelezo kuhusu kliniki na watoaji wa chanjo ya COVID-19 walio karibu nawe yanapatikana kwenye ukurasa wa [Vituo vya Chanjo ya COVID](#) wa NDDoH. Unaweza pia kupiga simu kwa Nambari Maalum ya NDDoH kupitia 1.866.207.2880 ili upate usaidizi.